Global Financial Integrity

Transparency International Kenya

# UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NCHINI KENYA




# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Uhamishaji wa fedha haramu ni nini? | 1 |
| Ufisadi | 2 |
| Kuna Uhusiano Gani | |
| Uuzaji wa Ethanoli Kimagendo | |
| Uuzaji Haramu wa Makaa | |
| Ufisadi Unakandamiza | |
| Umiliki Halisi | 7 |
| Kuna Uhusiano Gani | |
| Huduma ya Kitaifa ya Vijana(NYS) | |
| Sakata ya Anglo Leasing | |
| Sakata ya Goldenberg | |
| Usawa wa Kijinsia | 12 |
| Kuna Uhusiano Gani | |
| Usafirishaji Haramu wa Binadamu | |
| Huduma Bora za Kiafya | |
| Mazingira Bora | 17 |
| Kuna Uhusiano Gani | |
| Uwindaji Haramu | |
| Uvuvi Haramu | |
| Ukataji Haramu wa Miti | |
| Stakabadhi ghushi | 22 |
| Topolojia ya utumizi wa stakabadhi ghushi | |
| Sakata la Goldenberg | |
| Kesi ya Kahawa | |
| Mpango wa Nakumatt wa kutumia stakabadhi ghushi | |
| Kumbukumbu | 32 |

# JE, UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NI NINI?

Uhamishaji wa fedha haramu ni njia ambazo fedha au rasilimali hutumiwa ili kutoka nchi moja hadi nyingine.






Uhamishaji huu wa fedha haramu huathiri usalama wa nchi kwa kudhoofisha taasisi za kiserikali, kuathiri utekelezaji wa mifumo bora ya kisheria, na kusababisha nchi kukosa uwezo wa kupambana na umaskini.


Fedha haramu hupatikana kwa njia kama ufisadi, uhalifu uliopangwa, ukwepaji kodi, uwindaji haramu, na pia kuuza madini kwa njia za magendo.






# UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NA

# UFISADI



# Je kuna uhusiano upi baina ya uhamishaji wa fedha haramu na ufisadi hapa nchini Kenya?


1.




Fedha ambazo hupatikana kwa njia ya ufisadi mara nyingi huhitaji kufichwa. Kuhamishwa kutoka nchini ni njia mojawapo inayotumika kuzificha.


2.

Ufisadi pia hudhoofisha mbinu za kisheria ambazo zaweza kutumika kupunguza uhamishaji wa fedha haramu.




3.

Vikundi haramu hutumia ufisadi kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria na kuficha mapato ya biashara haramu kawa uuzaji haramu wa pembe za ndovu.



4.




Ufisadi pia hudhoofisha mfumo wa kisheria ambao unaweza kutumika kuwajibisha wale wanaotekeleza biashara haramu.

# Uuzaji wa Ethanoli kwa njia ya kimagendo




Uuzaji haramu wa ethanoli ambayo hutumika kwa kutengeneza pombe haramu imeongezeka nchini Kenya. Serikali hupoteza takribani shilingi bilioni thelathini kama ushuru kila mwaka kwa biashara hii haramu ya Ethanoli.[1] Askari na maafisa wengine wa kiserikali hupokea hongo ili kutochukulia hatua wahusika wakuu wa usafirishaji wa ethanoli haramu.[2]










Mfanya biashara mmoja kutoka nchini Kenya aliratibishwa kwa orodha ya waliosajili makampuni katika nchi ya Panama. Mfanyabiashara huyu pia anashukiwa kuwa mlanguzi mkubwa wa ethanoli. Mfanyabiashara huyu alisajiliwa kama mwenyehisa mkuu katika kampuni kwa jina Belgravia services.[3] Kampuni hii ina uhusiano wa karibu na nyingine kwa jina Africa Spirits limited ambayo ilipatikana na ethanoli haramu ya dhamana ya takribani shilingi bilioni moja katika kiwanda chao.[4] Mfanyabiashara huyu pia alipatikana na stempu bandia za Mamlaka ya ushuru hapa nchini. Hili limepelekea kuchunguzwa kwake kwa ukwepaji kodi wa takribani shilingi bilioni arobaini.[5]









# Uuzaji haramu wa makaa huchangia uhalifu

Kila mwezi makaa ya dhamana ya takribani shilingi milioni mia moja arobaini (140 million) huuzwa kimagendo kutoka nchini Kenya. Kikundi haramu cha alshabab kimeshukiwa kuhusika pakubwa katika biashara hii haramu ya makaa. Alshabab pia imehusishwa na vitendo vya kigaidi hapa nchini Kenya. Ripoti zimeonyesha kwamba wanajeshi wa Kenya wamehusishwa katika biashara hii haramu.[6]





Kikundi cha ugaidi cha Alshabab hupata mapato makubwa kutoka kwa ulanguzi haramu wa makaa. Kikundi hiki hutumia mji wa Kismayo ulio na bandari ili kufanikisha shughuli zao za kibiashara. La kushangaza ni kwamba mji wa Kismayo umekuwa katika ulinzi wa jeshi la Kenya kwa miaka mingi. Wanajeshi hawa wameshukiwa kwa kuhusika na biashara haramu ya makaa na kupokea hongo ya shilingi mia mbili kwa kila mfuko wa makaa unaouzwa. Mapato kutoka kwa biashara hii haramu inakisiwa kufika shilingi bilioni mbili kila mwaka.[7]

# UFISADI UNAKANDAMIZA




Kenya imeripotiwa kama nchi mojawapo yenye ufisadi wa hali ya juu.[8] Kila mwaka Kenya hupoteza shilingi bilioni mia mbili na sabini kwa sababu ya ufisadi. Hii ni takribani asilimia ishirini na tano hadi thelathini ya bajeti ya kila mwaka (25% - 30%).[9] Hili limefanya uchumi wa nchi kuzorota na pia kufanya miradi ya umma isikamilike.







Maafisa wa kiserikali hutumia majina ya wateuliwa na makampuni yasiyo na ofisi wala wafanyakazi ili kusafirisha pesa haramu kutoka Kenya hadi nchi zingine ambako itahalalishwa. Marehemu Rais Moi na marafiki zake walishukiwa kutumia wateuliwa na makampuni yasiyo na ofisi wala wafanyakazi katika mpango wa kusafirisha pesa kutoka nchini Kenya na kuekeza katika nchi za kigeni.[10] Afisa mmoja aliyekuwa mkurugenzi wa shirika la kusambaza umeme kwa jina Samuel Gichuru alitambulika kuwa mmiliki halisi wa fedha ambazo zilikuwa zimelipwa kama hongo kwa kandarasi ambazo serikali ilikuwa imepatiana. Fedha hizi zilinaswa kwenye akaunti iliyokuwa nchi ya kigeni.[11]




# UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NA
# UMILIKI HALISI









## Umiliki halisi wa kampuni au shirika ni nini?





Mmiliki halisi wa shirika au kampuni ni binadamu au mtu binafsi ambaye haswa anamiliki au kunufaika kiuchumi kutoka kwa shirika au kampuni. Ukweli kuhusu umiliki wa kampuni unapofichwa, hili laweza kusaidia kampuni kutumika katika biashara haramu.


## Je, kuna uhusiano upi kati ya uhamishaji wa fedha haramu na umiliki halisi wa makampuni?



Uhamishaji wa fedha haramu mara nyingi hutumia makampuni na mashirika yanayobuniwa ili kuficha wale wanaonufaika kutoka kwa fedha hizi.



Sheria zinazonuia kufichua mmiliki halisi wa kampuni, shirika au fedha zaweza kutumika kupunguza uhamishaji wa fedha haramu. Hii ni kwa sababu sheria hizi hufichua wale ambao huficha maelezo yao kutoka kwa vitengo vya kiserikali vinavyohusika katika uchunguzi wa fedha haramu.




- Mnamo mwaka wa 2017, sheria ya usajili wa makampuni ilibadilishwa na kuongezwa vipengele vinavyohitaji shirika au kampuni yoyote irekodi habari za umiliki wake.

- Baadaye, mwezi wa pili mwaka wa 2020, serikali ikapitisha kanuni za udhibiti wa umiliki halisi wa makampuni kama njia mojawapo ya kutekeleza sheria ya usajili wa makampuni.

Kwa mujibu wa sheria hizi, mashirika na kampuni zote zinahitajika kuwasilisha rejista ya wamiliki halisi kwenye ofisi ya msajili wa makampuni.

## Je, Kuna umuhimu upi kwa shirika au kampuni kuwa na Rejista ya wamiliki Halisi?


- Kusaidia kupunguza ufisadi, ukwepaji wa kodi, ufadhili wa ugaidi na utumizi wa makampuni yasiyo na ofisi wala wafanyakazi






- Kusaidia vitengo vya kiserikali katika uchunguzi.

- Kusaidia kuimarisha uwazi katika maswala ya kifedha nchini



# HUDUMA YA KITAIFA YA VIJANA (NYS)




Kwa muda wa miaka mitatu kutoka mwaka wa 2015, takribani shilingi bilioni kumi (10.5 billion) ziliibiwa kutoka kwa huduma ya vijana. Uchunguzi uliashiria ya kwamba wizi huu ulifanyika kutumia ankara ghushi na malipo zaidi ya mara moja kwa muuzaji mmoja. Kwa mfano, NYS ililipa muuzaji mmoja wa nyama takribani shilingi milioni kumi (10 million) kwa mwaka mmoja kama malipo ya kuuziwa nyama ya ngombe. Hii ni kusema kwamba vijana waliokuwa wameajiriwa mwaka huo walitarajiwa kula nyama kiasi cha kilo 66 kila siku. Makampuni mengine yaliyohusika katika sakata hii yalikuwa yamesajiliwa masaa kidogo tu kabla ya kupokea mamilioni ya pesa kwenye akaunti. Maafisa wa NYS walitumia makampuni haya kama njia ya kujificha wasitambulike kwa kutekeleza uporaji huu.









# SAKATA YA ANGLO LEASING




Miaka kama ishirini iliyopita, serikali ya Kenya iliipatia kampuni moja kwa jina Anglo leasing kandarasi ya kuchapisha pasipoti mpya. Stakabadhi hizi hazikuwasilishwa na serikali ilihadaiwa kwa kutumia mashirika yaliyokuwa bila ofisi wala wafanyakazi wowote.




Kamati ya bunge inayoangazia hesabu za umma iliripoti kwamba wizi huu ulitekelezwa kwa kutumia mipango ya hila. Kandarasi zote zilizokuwa kwenye sakata hii zilikuwa kumi na nane na zilikuwa na thamani ya takribani shilingi bilioni hamsini na tano (55 billion).

Uchunguzi unaashiria kwamba waliohusika walitumia hila kujificha wasitambulike lakini walikuwa wanamiliki makampuni kadhaa yaliyohusika.











# SAKATA YA GOLDENBERG




Miaka ya tisini (1990's), nchi ya Kenya ilikumbwa na uhaba wa fedha za kigeni. Katika mbinu mojawapo ya kurekebisha tatizo hili, serikali ilianzisha mfumo wa kuimarisha uuzaji wa bidhaa kutoka nchini hadi nchi za kigeni. Wanabiashara waliohusika katika biashara na nchi za kigeni waliongezewa asilimia ishirini (20%) ya mapato yao kama njia ya kuwapa motisha kuendelea na biashara.





Kampuni moja kwa jina Goldenberg iliyokuwa ikimilikiwa na wanabiashara kwa majina Kamlesh Pattni na James Kanyotu, mkurugenzi wa idara ya ujasusi ilianza uuzaji wa dhahabu na almasi katika mfumo huu. Lakini kwa kutumia mbinu ya kuhadaa serikali, kampuni hii ilitoa habari za uongo kwamba ilikuwa imeuza dhahabu na almasi ili kupokea malipo ya motisha kutoka kwa serikali.





Tume iliyoongozwa na jaji Bosire, iliyochunguza sakata hii, iliripoti ya kwamba Kenya ilipoteza takribani asilimia kumi (10%) ya mapato ya taifa katika sakata hii. Ripoti ya tume hii pia ilionyesha kwamba watu waliokuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa waliohusika katika sakata hii waliteua wasimamizi wa mbadala na stakabadhi ghushi wakati wa usajili ili kuhakikisha kwamba hawangetambulika kwa urahisi.






# UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NA

# USAWA WA KIJINSIA



# Je uhamishaji wa fedha haramu una uhusiano upi na usawa wa kijinsia?


Uhamishaji wa fedha haramu hupunguza kiwango cha fedha za umma ambazo zinaweza kutumika kuimarisha utoaji wa huduma bora. Ukosefu wa huduma bora huathiri usawa wa kijinsia.







Serikali inapopoteza hela kwa usafirishaji haramu, mara nyingi huwa inaongezea ada inayotozwa bidhaa muhimu za kila siku kama vyakula na dawa.

Wanawake nchini Kenya wanaathiriwa kwa kiasi kikubwa na ufisadi pamoja na uhalifu kama usafirishaji haramu wa binadamu ambao huchangia kwa kiasi kikubwa hela ambazo husafirishwa kwa njia haramu.




# Je uhamishaji wa fedha haramu huathiri haki za kijinsia vipi?[1]

Shirika la GFI linakadiria kwamba katika mwaka wa 2013, nchi ya Kenya ilipoteza takribani asilimia nane ya mapato yote ya kiserekali kwa sababu ya hila za kibiashara kama kutumia ankara za uongo.[2] Tukitumia takwimu za hivi karibuni, Kenya huenda ilipoteza takribani bilioni mia moja ishirini katika mwaka wa kifedha wa 2018-2019.




Hela zinazokadiriwa kupotea kila mwaka zimezidi shillingi bilioni tisini ambazo serikali ilitenga kwa maswala ya kiafya nchini na pia ni mara tatu ya shilingi bilioni arobaini na nne ambazo serikali ilitenga kwa miradi ya kulinda jamii.[3]





Serikali inapopoteza ushuru kutoka kwa ada inayotozwa mishahara na bidhaa za kutoka nchi za kigeni, utafiti unaonyesha ya kwamba serikali hupandisha ada inayotozwa bidhaa muhimu zinazonunuliwa na wananchi kila wakati kama vyakula. Ada ya vyakula na bidhaa za muhimu huenda ikaathiri wanawake zaidi ya wanaume. Hii ni kwa sababu wanawake mara nyingi huwa wana jukumu la kuimarisha afya, malezi na elimu ya jamii zao na kwa hivyo hununua bidhaa kama vyakula, dawa na vitabu.[4] Kwa mfano, katika mwaka wa kifedha 2018 -2019, ingawaje ushuru unaotozwa bidhaa za kutoka nje ya nchi ulipanda kwa asilimia tisa pekee, ada inayotozwa bidhaa nchini ilipanda kwa asilimimia kumi na mbili katika mwaka huo huo.



# Usafirishaji haramu wa binadamu huathiri usawa wa kijinsia


Utafiti wa shirika la GFI unaonyesha kwamba duniani kote, usafirishaji haramu wa binadamu ni biashara haramu kubwa inayozaa zaidi ya shilingi trilioni kumi na sita kila mwaka (takriban dola bilioni mia moja hamsini).[5] Biashara hii haramu huwaathiri kina mama na watoto zaidi. Nchi ya Kenya pia imeonyeshwa kuwa na visa vingi vya watu wanaotolewa, wanoletwa ama kupitishwa nchini kwa njia za hila.[6]




Katika mwaka wa 2019, serikali ya Kenya iliripoti visa vya usafirishaji haramu wa binadamu mia nane hamsini na tatu (853) ikiwemo wanawake mia sita ishirini na sita (626) na wanaume mia mbili ishirini na saba (227).[7] Takwimu hizi zinajumuisha wanawake waliosafarishwa kwa njia ya haramu kutoka nchi za kigeni kama India na Nepal na kuletwa nchini Kenya na pia waliosafirishwa kwa haramu kutoka nchini Kenya.[8] Ujuzi wa kisasa kuhusu maswala ya kifedha unaweza kutumika na serikali kuyafikia malengo yake ya kimaendeleo na pia kupunguza visa vya dhuluma ya kijinsia. Ujuzi huu wa kisasa wa maswala ya kifedha kama uwezo wa kutambua wanaomiliki biashara, makampuni na akaunti za benki unaweza kutumika na serikali kupambana na vikundi vya wahalifu vinavyotumia hila kutakatisha fedha haramu.[9]

# Uhamishaji wa fedha haramu huathiri uwezo wa serikali kutoa huduma bora za kiafya

Hapa nchini Kenya, sekta ambazo hupokea mgao mkubwa zaidi katika ugavi wa kila mwaka ndizo sekta ambazo pia hukumbwa na sakata za ufisadi kila wakati.[10] Katika mwaka wa kifedha wa 2015 - 2016, wizara ya afya ilipoteza takriban shilingi bilioni tano katika sakata iliyohusisha kampuni moja kwa jina Estama Investment Limited.[11] Hizi hela zilikuwa asilimia ishirini na moja (21%) ya mgao wa fedha ambao wizara ilipokea mwaka huo. Katika mwaka huo, shilingi milioni mia nane themanini na tisa zilinuiwa kutumika katika kuimarisha mpango wa kina mama kujifungua bila malipo katika hospitali za kiserekali.[12]





Kampuni ya Estama Investment ilipata kandarasi ya kuuzia serikali kliniki mia moja ambazo zingeweza kuhamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine. Ingawaje kampuni hii ilipokea malipo kwa kandarasi hii, hakuna kliniki yoyote iliyoletwa kwa mikono ya serikali. Kampuni ya Estama pia ilikuwa imeficha maelezo ya umiliki wake na kwa hivyo waliotekeleza ufisadi huu hawajakamatwa mpaka wa leo.[13] Uchunguzi wa tume ya maadili na kupambana na ufisadi (EACC) imeashiria ya kwamba kulikuwa na uhusiano wa karibu kati ya maafisa wa wizara ya afya na wanao shukiwa kusajili kampuni ya Estama investments Limited.[14] Kutoweza kuwatambua washukiwa wakuu wa sakata hii ya ufisadi kulisababisha serikali kupoteza fedha ambazo zingetumika kuimarisha huduma bora kwa wananchi haswa walio hatarini kama watoto na akina mama.



# UHAMISHAJI WA FEDHA HARAMU NA

# MAZINGIRA BORA



# Je kuna uhusiano upi baina ya uhamishaji Wa Fedha Haramu Na Maswala Ya Mazingira Bora Nchini Kenya?





Nchi ya Kenya imebarikiwa na maliasili kama mafuta, misitu, Wanyama pori na pia samaki wa aina mbalimbali. Wananchi wengi hupata riziki yao kwa kutumia maliasili hizi. Hata hivyo, maliasili hizi pia hutumiwa na vikundi haramu, vikundi vya kujihami na mashirika ya kuendesha biashara haramu kujinufaisha.




Walio na haki na wale wanaotumia maliasili kwa njia za hila wote hung'ang'ania raslimali hizi kujinufaisha kibinafsi. Katika kutafuta manufaa ya kibinafsi, wengine hutumia kemikali hatari ilhali wengine hutumia udanganyifu na hila ili kusafirisha mapato yanayotokana na maliasili kinyume na sheria.



# Uwindaji Haramu

Nchi ya Kenya imebarikiwa na wanyama wa kila aina. Hata hivyo kuna raia wa nchi za kigeni ambao wana hamu kubwa ya kununua pembe za ndovu na vifaru. Hii hamu huwa inachangia vikubwa kuenea kwa uwindaji haramu na usafirishaji haramu wa pembe hizo. Biashara hii haramu inakisiwa kuleta mapato ya fedha haramu takribani shilingi bilioni tano hadi bilioni ishirini na tatu (5 - 23) kila mwaka. Hili limefanya uwindaji haramu kuwa mojawapo ya biashara haramu zenye mapato makubwa zaidi duniani kote.[1] Kati ya mwaka wa 2007 hadi 2017, nchi ya Kenya iliripoti visa zaidi ya mia saba tisaini na saba za pembe za ndovu zilizonaswa zikisafirishwa. Kenya ilikuwa imeongoza ikilinganishwa na mataifa mengine Afrika na hata duniani kote.[2]

Mnamo mwaka wa 2015, takribani tani sita za pembe za ndovu zilisafirishwa kutoka bandarini Mombasa kelekea Hongkong na Singapore ambako zilinaswa. Uchunguzi zaidi ulionyesha kwamba kikundi kikubwa cha wahalifu kilihusika katika mradi huu wa kificha pembe za ndovu ili zifikiriwe kuwa bidhaa za kawaida za kibiashara. Kikundi hiki kilikuwa kimesajili kampuni ya uuzaji wa majani chai ambayo waliitumia kununua majani chai alafu baadaye kupakia pembe za ndovu katika mifuko ya majani chai ili kuhadaa maafisa wa bandari.[3]






# Uvuvi Haramu


Taasisi ya utafiti wa maswala ya uvuvi hapa nchini imekisia ya kwamba nchi ya Kenya hupoteza takribani shillingi billioni kumi kila mwaka kwa uvuvi haramu unaotekelezwa na mashirika ya kigeni.[4]

Uvuvi haramu hudhoofisha uvuvi halali ambao huleta manufaa kwa wananchi wa kawaida. Uvuvi haramu pia umehusishwa na kuchangia maovu mengine kama utapeli, usafirishaji haramu wa binadamu, silaha na madawa ya kulevya.


Katika kesi moja, meli mbili zilizokuwa zinaendeleza uvuvi katika pwani ya Kenya na Somalia ziligunduliwa kwamba hazikuwa na leseni ya uvuvi.

Katika shughuli za uchunguzi zaidi, meli hizo zilishukiwa kuendeleza biashara haramu ya uuzaji baharini. Meli moja kwa jina Poseidon, ilikuwa haina samaki wowote kwenye meli ingawaje ilikuwa baharini kwa muda wa zaidi ya wiki sita.

Raia mmoja wa kutoka Korea kusini alitumika kama msimamizi wa wamiliki halisi wa meli hizo na kwa hivo ikawa vigumu kutambua wamiliki haswa waliokuwa wakinufaika na biashara hii haramu.[5]



# Ukataji haramu wa miti




Ukataji wa miti kiholela umekuwa kero kubwa hapa nchini haswa kwa kuharibu mazingira. Ukataji haramu wa miti husababisha kupungua kwa misitu nchini kwa kiasi cha ekari elfu saba kila mwaka. Nchi ya Kenya pia hutumika kama njia ya kusafirisha mbao na miti iliyokatwa kwa njia ya haramu kutoka nchi jirani. Makundi haramu hutumia hongo ili kukwepa mkono wa sheria. Makundi ya kijamii ya kulinda misitu pia yametumika kusaidia vikundi haramu vinavyokata na kusafirisha miti.[6]




Mti wa msandali au sandalwood unapatikana kwa viwango vya juu katika kaunti ya Samburu. Hili limefanya makundi haramu ikiwemo wafanyi biashara na maafisa wa serikali kujihusisha na biashara haramu ya ukataji na usafirishaji wa miti hii. Vikundi hivi husafirisha miti ya msandali hadi nchi ya Uganda na kutumia viwanja vya ndege au konteina za barabarani kusafirisha miti hii hadi nchi za nje. Mfanyibiashara mmoja amekuwa akitumia hongo kupata leseni ya kusafirisha mbao hizi kutoka kwa maafisa wa kulinda misitu.[7]




UHAMISHAJI WA FEDHA NA

# UTUMIZI WA STAKABADHI GHUSHI KWENYE BIASHARA



# JE! UTUMIZI WA STAKABADHI GHUSHI KATIKA BIASHARA KUHAMISHA FEDHA HARAMU HUFANYIKA VIPI?



Utumizi wa stakabadhi ghushi ni njia mojawapo inayotumika kuhamisha fedha haramu


Thamani iliyonakiliwa kwenye ankara ya bidhaa zinazouzwa nje na ndani ya nchi zinaweza kubadilishwa ili kuficha dhamana halisi ya biashara.







GFI inakadiria kwamba mwaka wa 2017, Kenya ilipoteza shilingi bilioni 95 kwa mtiririko haramu wa fedha kutokana na utumizi wa stakabadhi ghushi.


## TOPOLOJIA YA UTUMIZI WA STAKABADHI GHUSHI KWENYE BIASHARA.



# SAKATA LA GOLDENBERG





Katika miaka ya 1990, akiba ya fedha za kigeni za Kenya zilikuwa zimepungua. Kuhimiza mapato ya fedha za kigeni, serikali ya Kenya ilianzisha mpango wa kukuza mauzo ya nje ambapo wauzaji nje ambao walioweka mapato yao kwenye akaunti wangepokea pesa sawia na walizoweka na pia motisha wa ziada wa asilimia 20% .








Kampuni ya Goldenberg International Ltd ilishirikiana na maafisa wa serikali kutumia vibaya mfumo huu katika kusafirisha dhahabu na almasi, wakikubaliana kuwa kampuni hiyo italipwa fidia ya kuuza nje ya aslimia 35% - 15% juu ya kiwango halali. Kwa kuwa Kenya haikuwa na almasi na dhahabu tosha toka nchini, kampuni hiyo ilitangaza kuuza nje dhahabu na almasi kwa uwongo na ikatoa noti bandia za sarafu ngumu kudai fidia hiyo.[1]



# KESI YA KAHAWA

Kampuni ya Kenya SMS Ltd, ilionekana kwenye faili za FinCEN kwa sababu ya malipo yasiyoeleweka kutoka kwa wafanyabiashara wa kahawa wa Kenya . Licha ya kujulikana na benki ya Marekani kuwa iko katika biashara ya uuzaji wa dawa na bidhaa za matibabu, SMS Ltd ilipokea shilingi milioni 36 (US$ 3.3 million) kwa mauzo ya kahawa kwa mashirika ya Kenya. Kampuni hii inashirikiana na wakurugenzi na wamiliki wa kampuni zinazohusiana na familia ya Kenyatta.




Kwa kuongezea, SMS Ltd ilipokea shilingi milioni 76 (US$ 7 million) kutoka kwa kampuni ya uzalishaji wa mafuta ya mboga iliyoko Dubai kwa ununuzi wa runinga na mashine za DVD. Mmiliki wa faida wa biashara za tuhuma na malipo haya hajulikani: SMS Ltd inamilikiwa na kampuni iliyosajiliwa Delaware, jimbo linalojulikana kwa usiri wa mashirika.[2]

# MPANGO WA NAKUMATT WA KUTUMIA STAKABADHI GHUSHI

Lililokuwa shirika bora la maduka makubwa ya uuzaji wa bidhaa Afrika ya Mashariki, Nakumatt ya Kenya ilidaiwa kuendesha mpango mkubwa wa biashara pana za kitapeli kabla ya kufilisika mwaka wa 2020. Kwa kuanzisha mtandao ulio wazi wa biashara zinazohusiana, ambazo zinafanya biashara kati yao, mabilioni ya pesa yanaweza kuhamishwa ndani na nje ya nchi kwa kuficha malipo ya pesa kama malipo kwa wauzaji halali wanaotumia ankara bandia.







Mtandao wa Nakumatt ulitumia akaunti za mteja wa wakili kwa mazoezi haya ya utangazaji mbaya wa biashara.Kwa kuwa akaunti ya aina hii inalinda na usiri wa mteja na imefutwa kutoka kwa kufuata Sheria ya Mapato ya Uhalifu na Kupambana na Utapeli wa Fedha ya Kenya au kukaguliwa na Mamlaka ya Mapato ya Kenya, Uhamishaji huo wa fedha haramu ulibaki bila kutambuliwa kwa karibu miaka thelathini.[3]






# MAPENDEKEZO

1. Mashirika ya Kijamii
Mashirika ya kijamii yanaweza kushirikiana kuangazia uhusiano kati ya uhamishaji wa fedha haramu na: ufisadi; umiliki halisi; usawa wa jinsia; na haki ya mazingira bora, ili kutetea kuimarishwa kwa mfumo wa kifedha nchini.





2. Kubuni na kutekeleza sera imara za kiserikali za kupunguza uhamishaji wa fedha haramu.



a. Kutekeleza sheria mpya ya umiliki halisi wa makampuni na mashirika

b. Kurekebisha sheria ya umiliki halisi wa mashirika ili kuhakikisha kwamba mifumo yote ya usajili wa mashirika imezingatiwa katika sheria hii.





c. Kuweka rejista wazi ya umiliki wa makampuni.





d. Kuhakikisha kwamba idara ya usajili wa makampuni inakagua maelezo yanayotolewa na makampuni kuhusu wamiliki halisi.



e. Kupigia debe uwazi katika mfumo wa kifedha nchini.





f. Kuhakikisha kwamba wamiliki halisi wanatambuliwa wakati kampuni yoyote inaposajiliwa..




g. Kupigia debe kubadilishana kwa habari kati ya mataifa tofauti ili kuwatambua watekelezaji wa usafirishaji fedha haramu.

h. Kuchangia katika kutekelezwa kwa mkataba wa makubaliano kuhusu kurejeshwa kwa mali iliyoporwa kutoka hapa nchini.



i. Kuimarisha sheria zinazowalinda wanaoripoti ufisadi.




j. Kutekeleza sera ambazo zitapunguza utumizi wa stakabadhi ghushi katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa kutoka mataifa ya kigeni.

k. Kuchunguza zaidi shughuli za kibiashara zinazofanyika kati ya nchi ya Kenya na mataifa ambayo hayatozi kodi na pia kuficha habari kuhusu wamiliki ma akaunti za benki.






l. Kubuni ufafanuzi thabiti wa umiliki wa faida kwa wakala wote wa serikali




m. Idara ya Ushuru ya Kenya inapaswa kutoa adhabu inayofaa kwa kukosa kutoa habari za mmiliki halisi zilizo sahihi.


n. Katika siku za usoni, Tathmini za Kitaifa za hatari, kudokeza kanuni zinazoshughulikia njia za kupunguza matumizi mabaya ya njia za biashara ya ardhi, angani na baharini kwa madhumuni ya kutangaza biashara vibaya.



3.Kuimarisha uwazi katika mipango ya kibiashara

a. Kutekeleza sera ambazo zitapunguza utumizi wa stakabadhi ghushi katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa kutoka mataifa ya kigeni.



b. Kuchunguza zaidi shughuli za kibiashara zinazofanyika kati ya nchi ya Kenya na mataifa ambayo hayatozi kodi na pia kuficha habari kuhusu wamiliki ma akaunti za benki.

# KUMBUKUMBU


A. Ufisadi

1-https://eastafricamonitor.com/an-inside-job-kenyas-struggles-to-stop-ethanol-smuggling/

2-https://www.standardmedia.co.ke/business/article/2001320424/system-is-abetting-ethanol-smuggling-in-kenya

3-https://kenyainsights.com/forgotten-files-billionaire-humphrey-kariuki-busted-using-shell-companies-to-evade-tax-in-kenya/

4-https://www.the-star.co.ke/news/2019-02-09-state-closes-thika-brewer-over-tax-evasion-fake-liquor/

5-https://www.pulse.com.gh/bi/politics/cyprus-throws-kenyan-billionaire-humphrey-kariuki-under-the-bus-and-reconsiders-his/e0e0pcn

6-https://news.trust.org/item/20140326164355-aswmt

7-https://www.fairplanet.org/story/axis-of-evil-the-illegal-charcoal-trade-from-kenya-tothe-gulf-states/

8-https://www.transparency.org/en/cpi/2019/results/ken

9-https://magazine.vunela.com/corruption-development-and-governance-in-kenya-9036f3a0b681

10-https://www.theguardian.com/world/2007/aug/31/kenya.topstories3

11-https://star.worldbank.org/corruption-cases/sites/corruption-cases/files/Gichuru_Jersey_AG-v-Windward%20Trading%20Limited_2016_JRC_48A_24-Feb-2016.pdf

B. Umiliki Halisi

1-https://www.bbc.com/news/world-africa-44280453

2-https://www.dw.com/en/massive-corruption-case-grips-kenya-prosecution-charges-suspects/a-43964072

3-https://star.worldbank.org/corruption-cases/node/18486
https://www.theelephant.info/features/2019/09/05/tales-of-state-capture-goldenberganglo-leasing-and-eurobond/

4-http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/CommissionReports/Report-of-the-Judicial-Commission-of-Inquiry-into-the-Goldenberg-Affair

5-https://www.theelephant.info/features/2019/09/05/tales-of-state-capture-goldenberganglo-leasing-and-eurobond/

# KUMBUKUMBU


C. Usawa wa Kijinsia

1-https://www.u4.no/publications/the-gendered-dimensions-of-illicit-financial-flows

2-https://gfintegrity.org/report/kenya-potential-revenue-losses-associated-with-trade-misinvoicing/

3-https://www.treasury.go.ke/budget-statement-2018-19.html

4-https://www.oecd.org/dac/gender-development/44896295.pdf

5-https://gfintegrity.org/report/transnational-crime-and-the-developing-world/

6-https://www.state.gov/wp-content/uploads/2019/06/2019-Trafficking-in-Persons-Report.pdf

7-https://www.state.gov/reports/2020-trafficking-in-persons-report/kenya/

8-https://af.reuters.com/article/kenyaNews/idAFL8N24Y4XO

9-https://www.youtube.com/watch?v=DYZP7EA4I8E

10-https://tikenya.org/wp-content/uploads/2017/09/East-African-Bribery-Index-EABI-2017-1-1.pdf

11-https://trackcorruption.org/sh-5-billion-revealed-taxpayers-lose-sh5bn-innys-style-afya-house-theft/

12-https://data.unicef.org/resources/trends-maternal-mortality-2000-2017/

13-https://www.businessdailyafrica.com/bd/economy/revealed-taxpayers-lose-sh5bn-in-nys-style-afya-house-theft--2129568

14-https://www.standardmedia.co.ke/business-news/article/2001284601/eaccdeal-with-company-to-return-sh800m-for-clinics

# KUMBUKUMBU

D. Mazingira Bora

1-https://www.gfintegrity.org/wp-content/uploads/2017/03/Transnational_Crime-final.pdf

2-https://www.traffic.org/site/assets/files/12726/kenyas-ports-analysis-1.pdf

3-http://www.fatf-gafi.org/media/fatf/documents/Money-laundering-and-illegal-wildlife-trade.pdf

4-https://www.kmfri.co.ke/images/pdf/PSMA-Ratification-Advert.pdf

5-https://stopillegalfishing.com/wp-content/uploads/2017/03/Illegal-Fishing-Evidence-and-Analysis-WEB.pdf

6-https://www.theafricareport.com/16150/kenya-has-lost-nearly-half-its-forests-time-for-the-young-to-act/

7-https://www.voanews.com/africa/report-kenya-losing-forests-organized-crime

8-https://www.standardmedia.co.ke/kenya/article/2001276130/exposed-rogue-government-officers-fuelling-illegal-logging-trade

9-https://nation.africa/kenya/nation-prime/how-illegal-sandalwood-tradethrives-in-full-glare-of-authorities-278284

E. Stakabadhi ghushi

1-https://www.theelephant.info/features/2019/09/05/tales-of-state-capturegoldenberg-anglo-leasing-and-eurobond/

2-https://www.theelephant.info/data-stories/2020/09/28/kenya-transactions-infincen-files-raise-suspicions-around-coffee-and-ivory-trade/

3-https://newszetu.com/money-laundering-at-heart-of-nakumatts-downfall/

Kwa maswali ama ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana nasi:


**GLOBAL FINANCIAL INTEGRITY**
**(GFI)**
Mtu wa kuwasiliana naye:
Lakshmi Kumar - Mkurugenzi wa Sera
Pine Tree Plaza
Kaburu Drive 8th Floor
Kilimani, Nairobi
Email: lkumar@gfintegrity.org or gfi@gfintegrity.org

**TRANSPARENCY INTERNATIONAL - KENYA**
Mtu wa kuwasiliana naye:
Gerald Omumbo - Afisa Mtendaji wa Mawasiliano
Kindaruma Road, Off King Road
Next to Commodore Office Suites
Gate 713: Suite 4
Kilimani, Kenya
Tel: 254 (0) 202 727 763/5
Mobile: +254 703 247 825
Email: g.omumbo@tikenya.org or transparency@tikenya.org


GLOBAL FINANCIAL INTEGRITY

TRANSPARENCY INTERNATIONAL KENYA

Designed and illustrated by Thinkillustrate.